

HUDUMA ZA MLIMA WA MOTO NA MIUJIZA

Makao Makuu ya Kimataifa, Lagos, Nigeria.

NGUVU LAZIMA IBADILI MIKONO, RATIBA MAALUM YA MAOMBI YA MIKONO

KUPAMBANA NA MAPEPO WA JANGA (2)

APRILI 2022

Maandiko ya Kusoma: Zaburi 17; 27; 91

Ungamo: Zaburi 91

IBADA YA KUSIFU YA UCHOKOZI.

(IBADA MKALI YA KUSIFU)

1. Ee Mungu, inuka, ung'oe chochote Usichopanda ndani Mlima wa Moto na Miujiza, katika jina la Yesu.
2. Ee Mungu, acha moto wa uamsho ushuke juu ya Mlima wa moto na miujiza, kwa jina la Yesu.
3. Ee Mungu, acha nguvu ya amani na maendeleo, ifunike taifa hili, kwa jina la Yesu.
4. Ee Mungu, inuka na utupe viongozi wanaomcha Mungu, katika jina la Yesu.
5. Ninauzuia mwili wangu dhidi ya kila uvamizi wa watoto wa ajabu wa janga hili, kwa jina la Yesu.
6. Moto wa Roho Mtakatifu, choma amana zote za janga hili kutoka kwa mwili wangu, kwa jina la Yesu.
7. Damu ya Yesu, zua maisha yangu kutoka kwa kila roho ya tauni, kwa jina la Yesu.
8. Ninanyamazisha sauti ya watoto wa ajabu wa gonjwa wanaonena dhidi ya maisha yangu, katika jina la Yesu.
9. Damu ya Yesu, nipe chanjo dhidi ya kila udhaifu unaotokana na janga hili, katika jina la Yesu.
10. Mwili wangu, sikia neno la Bwana, kataa kila udhaifu, kwa jina la Yesu.
11. Sitakufa bali nitaishi kulitangaza Neno la Mungu katika majira haya, katika jina la Yesu.
12. Kila mshale wa janga, nililorushiwa, rudi kwa watumaji wako, katika jina la Yesu.

13. Wewe nguvu ya waharibifu, unaotokana na janga, mwili wangu sio mgombea wako, ondoka, kwa jina la Yesu.
14. Ngazi yoyote ya giza inayokaribisha mawakala wa pepo wa janga hili kwenye mwili wangu, vunjika, kwa jina la Yesu.
15. Ninapokea toniki na vitamini ya kiungu kwa nguvu katika damu ya Yesu, katika jina la Yesu.
16. Mfumo wangu wa kinga, pokea moto mpya na usiwe na upinzani na udhaifu wowote, katika jina la Yesu.
17. Kila nira na agano lililotengenezwa na janga hili, maisha yangu sio mgombea wako, vunjika, kwa jina la Yesu.
18. Kila mpango wa roho ya kifo kwa mwili wangu unaotokana na janga hili, uzimishwe, kwa jina la Yesu.
19. Ninasema ole ,kwa kila msumbu fu wa hatima yangu, katika jina la Yesu.
20. Ninafukuza kila ushawishi mbaya wa janga kutoka kwa mwili wangu, kwa jina la Yesu.
21. Kila nanga ya waharibifu, mwili wangu sio mgombea wako, kwisha, kwa jina la Yesu.
22. Roho Mtakatifu na uweza wa uvuli wa Mwenyezi, unifunike, katika jina la Yesu.
23. Ee Mungu, inuka na ufanye mwili wangu kuwa moto sana kwa kila pepo wa magonjwa, katika jina la Yesu.
24. Magonjwa ya umauti, yanayotokana na janga, mimi si mgombea wako, kufa, kwa jina la Yesu.
25. Mwili wangu, lisikie Neno la Bwana, usiwe chakula kwa walao nyama na wanywaji wa damu, kwa jina la Yesu.
26. Kinga ya Kiungu, nifunike na uniloweke, katika jina la Yesu.
27. Kila tatizo lililopangwa na watoto wa ajabu wa janga hili dhidi ya maisha yangu, libatilishwe, kwa jina la Yesu.
28. Kila unabii wa giza, maombi ya giza, matamanio ya giza dhidi ya ustawi wangu, tawanyika katika jina la Yesu.
29. Kila nyoka na nge wa roho ya tauni, ninakuponda, kwa jina la Yesu.

30. Damu ya Yesu, moto wa Roho Mtakatifu, takasa mwili, nafsi na roho yangu, katika jina la Yesu.
31. Kila nguvu iliyopewa kusumbua hatima yangu kunifanya nishindwe, ushindwe, katika jina la Yesu.
32. Nguvu ya Mungu, funika kila sehemu ya maisha yangu kwa uponyaji kamili na ukombozi, katika jina la Yesu.
33. Kila nira ya usumbufu, vilio na kizuizi iliyopangwa na janga dhidi ya maisha yangu, vunjika, kwa jina la Yesu.
34. Malaika wa vita mko wapi, inukeni na kunipigania katika majira haya, kwa jina la Yesu.
35. Mtu wangu wa roho, ujazwe na moto wa Roho Mtakatifu na ukatae kila mshale wa giza, kwa jina la Yesu.
36. Kila kitu kizuri nilichopoteza wakati wa janga hili, ninakimiliki tena, kwa jina la Yesu.
37. Kila mwandiko wa waovu uliopotoshwa wakati wa janga hili, ufutiliwe mbali kwa damu ya Yesu, katika jina la Yesu.
38. Roho Mtakatifu na moto ,jaza mwili, nafsi na roho yangu, katika jina la Yesu.
39. Kila sauti mbaya, inayonena dhidi ya damu yangu, ninakunyamazisha, kwa jina la Yesu.
40. Mkono wowote unaotaka kulipiza kisasi dhidi yangu, kwa sababu ya maombi yangu, nyauka kwa moto, kwa jina la Yesu.